# ILANI YA BINTI AFRIKA BEIJING+25

## FEM - KUZA. WEZESHA. HAMASISHA

Ilani hii ya Mtetezi wa Haki za Wanawake inaainisha madai Kwa ajili ya Jukwaa za Vizazi vya Usawa

Novemba 2020



# UTANGULIZI

Mwaka 2020 unatimiza maadhimisho ya miaka ishirini na mitano ya Kongamano la Nne Duniani la Wanawake na utumizi wa Azimio la Beijing na Jukwaa la Uamsho (1995). Kabla ya hapo, Mkutano wa 1 wa shirika la Umoja wa Mataifa (UN) Duniani kuhusu Wanawake ulifanyika huko Mexico mwaka wa 1975, katika kipindi cha Mwaka wa Wanawake wa Umoja wa Afrika Kimataifa. Mkutano huu ulikuwa wa kwanza kwa asili yake kulenga mahsusi masuala ya wanawake na uliweka alama ya mageuzi katika utengenezaji wa sera.

Shirika la Umoja wa Afrika liliitangaza miaka ya 1976 -1985 kuwa Mlongo wa Wanawake, ambao katika huo Mkutano wa 2 Kimataifa uliohusu Wanawake ulifanyika huko Copenhagen, Denmark mwaka wa 1980, na ulijikita zaidi katika kuimarisha mitandao ya wanawake. Mkutano wa 3 ulifanyika mjini Nairobi, Kenya mwaka wa 1985 na ulikamilisha Mlongo wa Umoja wa Arika kwa ajili ya Wanawake, na kutathmini maendeleo yaliyopatikana na utumizi wa "Mikakati ya Kusonga Mbele kwa ajili ya Maendeleo ya Wanawake". Mkutano huu ulikuwa msingi wa majadiliano ya Mkutano wa 4 wa Kimataifa kuhusu Wanawake uliofanyika jijini Beijing na kuacha mwongozo kuhusiana na uwezeshwaji wa wanawake na usawa wa jinsia.

2020 pia inatimiza maadhimisho ya miaka 20 ya Azimio la 1325 (S/RES/1325) juu ya wanawake, amani na usalama, lililothibitisha tena kwa mara nyingine umuhimu wa wanawake katika uzuizi wa migogoro na kusisitiza umuhimu wa ushiriki sawa na ujumuishwaji kikamilifu katika jitihada zote za kudumisha na kukuza amani na usalama.

Kwa bahati mbaya, licha ya hatua iliyofikiwa, hakuna nchi iliyoweza kufikia usawa wa kijinsia. Kwa kulizingatia hili, taasisi za jamii pamoja na Wanawake wa Umoja wa Afrika wamezindua kampeni ya: "Kizazi cha Usawa: Utambuzi wa haki za wanawake kwa ajili ya Usawa siku za mbeleni", iliyolenga kukutanisha vizazi vya wanaharakati wa haki za wanawake kushughulikia suala hili la uwezeshwaji wa wanawake ambalo bado halijakamilika.




ILANI YA BINTI
AFRIKA BEIJING+25

Uzinduzi wa kampeni hii umesababisha utengenezwaji wa Jukwaa la Kizazi cha Usawa (GEF) ambalo litaendesha mkutano wa kimataifa kwa ajili ya usawa wa wanawake, utakaoitishwa na Wanawake wa Umoja wa Mataifa na kusimamiwa na Ufaransa pamoja na Mexico, kwa kushirikiana na asasi za kiraia. Kutokana na mlipuko wa janga la COVID-19, GEF imehairishwa hadi 2021. Mfumo wa utekelezaji wa GEF uliahidi kujengwa katika msingi wa kanuni za ujumuishaji, na mkakati wa kwanzia chini kuelekea juu, ulioundwa katika msingi wa kujumuisha nguvu kwa pamoja, katika ushirikiano wa kimataifa, wenye wadau wengi, uliolenga kuhamasisha serikali, jamii, taasisi za kimataifa na sekta binafsi.

Ndani ya ngazi ya bara la Afrika; katika Mkutano Usio wa Kawaida wa Mawaziri wa Jinsia na Masuala ya Wanawake huko Maseru, Lesotho Desemba 2008, Shirika la Umoja wa Afrika (AU) Mawaziri wa Jinsia na Masuala ya Wanawake walilitaka Shirika la Umoja wa Afrika kutangaza miaka ya 2010-2020 kuwa Mlongo wa Wanawake wa Afrika uliopitishwa na Mkutano wa Desemba. 487 (XIX) chini ya Kichwa cha Mada: Mbinu Msingi za Usawa wa Jinsia na Uwezeshwaji wa Wanawake.

Jitihada hii madhubuti imeingizwa katika azimio la mlongo mpya (2020-2030) wa Ujumuishwaji wa Wanawake katika Masuala ya Fedha na Uchumi, lililowekwa na viongozi wa Afrika mwezi Februari mwaka wa 2020. Azimio hili ni matokeo ya dhamira ya viongozi wa Afrika kuimarisha hatua za ujumuishwaji endelevu wa kijinsia katika maendeleo endelevu ya ngazi za kitaifa, kikanda na kibara. 2020 pia imetimiza maudhui ya mwaka ya Umoja wa Afrika ya "Unyamazishaji wa Bunduki: Utengenezaji wa Mazingira Rafiki kwa ajili ya Maendeleo ya Afrika" yaliyoamuliwa na Baraza la Watendaji kipindi cha Kilele cha Ushirikiano wa Umoja wa Afrika huko Niamey, Niger, Julai 2019 na kutumika kipindi cha 33 cha Kilele cha Umoja wa Afrika, jijini Addis Ababa Februari 2020.

Katika kusheherekea hatua hizi, mifumo ya vijana ni funguo wa kuimarisha haki za vijana zinazojumuisha, ila zisizozuiwa tu katika, "Uwekezaji katika Vijana kwa ajili ya Kunufaika katika Mgao wa Idadi ya Watu", maudhui ya mwaka 2017 ya Umoja wa Ulaya, Kampeni ya Vijana katika Unyamazishaji wa Bunduki mwaka 2020, Mfumo wa Vijana katika ngazi ya Bara, Amani na Usalama, na Azimio la Vijana wa Afrika katika Kunyamazisha Bunduki.




ILANI YA BINTI
AFRIKA BEIJING+25

Makala ya 23 ya Katiba ya Vijana wa Afrika, inazungumzia mahsusi *Wasichana na Mabinti*, kwa kuitisha ulinzi wa wasichana na mabinti dhidi ya unyonywaji wa kiuchumi na ufanyaji wa kazi hatarishi, zinazowaondoa kutoka mashuleni ama zinazoweza kudhuru afya yao ya kiakili na kimwili. Chapisho la **Sauti صوتي** la Umoja wa Afrika limeelezea zaidi changamoto hizi kutoka kwenye nyanja za kiuchumi, kitamaduni na kisiasa hadi katika utengwaji wa mabinti katika sera za vijana na wanawake, sekta na mifumo, unaopelekea changamoto zao mahsusi kutoshughulikiwa. Janga la sasa la COVID-19 limezidisha changamoto hizi zinazowakumba mabinti; kwanzia kwenye suala la ugumu wa kiuchumi hadi katika ukatishwaji wa shule na matumizi mabaya ya vipindi vya kujifungia ndani kama ilivyoainishwa katika chapisho la sera ya Uongozi wa Vijana Afrika "Taarifa Halisi & Takwimu za Changamoto za Uwakala wa Vijana wa Afrika na Mpango wa Urejeshi baada ya COVID-19".

Hivyo, ilani hii ya Mabinti wa Afrika ni nyaraka ya kisiasa inayoainisha masuala muhimu yahusuyo mabinti wa Afrika na kuweka madai ya kushughulikia masuala hayo. Ilani hii ni matokeo ya Mabaraza 5 ya Kikanda ya Mabinti wa Afrika Beijing+25 yaliyojumuisha zaidi ya washiriki 1500 na zaidi ya wanachama 30 wenye malengo ya **FEM**:

## KUZA

uongozi ujumuishao vizazi mbalimbali, na mahojiano miongoni mwa wanawake, wadau wa Mashirika ya Umoja wa Afika na Umoja wa Mataifa

## WEZESHA

mabinti katika kanda tofauti tofauti kushirikisha mapendekezo yao na kushirikishwa katika ngazi za kijamii, kitaifa, kikanda na kibara

## HAMASISHA

ilani hii ya Mabinti wa Afrika yenye madai 10 ya utendaji

Hivyo, ilani hii hutoa jukwaa la madai ya pamoja ya kufikia usawa wa kijinsia pamoja na Ajenda ya 2063 na Ajenda ya 2030. Huwezesha mabinti kueleza masuala yao na kulinda dhamira angavu na ya wazi, Jukwaa la Kizazi cha Usawa na Uongozi wa Utendaji wa pamoja, ambazo huweka alama katika sera zilizopo, michakato ya kitaasisi, na mikakati na programu za ujumla. Madai haya yatahakikisha kwamba wasichana na mabinti wanaweza kushiriki kiamilifu, kwa usawa na kwa ufanisi, kwenye ngazi zote za kijamii, kielimu, kisiasa, kitamaduni, maisha ya kiraia na uongozi pamoja na jitihada za kisayansi.

Mchakato wa kutengeneza na kuhamasisha ilani hii umezingatia pia mapitio ya mabinti, jambo linalohakikisha kuwa ilani hii itaweza kumilikiwa na wigo mpana wa kikatiba. Hivyo mabinti huwezeshwa kutumia sauti zao kuleta vijana wengi zaidi katika harakati hii. Washiriki wa kanda tano za majadiliano wametokea nchi 45, ambazo ni **Algeria, Angola, Benin, Botswana, Burkina Faso, Kameruni, Chad, Côte D'Ivoire, Visiwa vya Komoro, Kongo, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Djibouti, Eswatini, Misri, Ethiopia, Eritrea, Ghana, Gambia, Kenya, Liberia, Libya, Lesotho, Malawi, Mozambique, Morocco, Mauritania, Madagaska, Mauritius, Namibia, Nigeria, Rwanda, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kiarabu ya Sahrawi, Afrika Kusini, Sierra Leone, Senegal, Somalia, Sudani Kusini, Sudani, Tanzania, Tunisia, Togo, Uganda, Zimbabwe, na Zambia.**

# DAI LA HAKI YA KIUCHUMI

**Sisi, Mabinti wa Afrika, tunadai:**

- Usawa katika kazi, ajira zinazoheshimika, kazi yenye ujira, mafunzo ya kazi yenye ujira na mishahara sawa katika ujira wa lisaa, kwenye ajira za nusu muda na ajira za muda kamili, katika hali zinazofanana. Kwanini tulazimike kuweka juhudi mara mbili ili tu kuonyesha kwamba tunaweza? Malipo pungufu kwa wanawake yanamaanisha kuwa sisi tuna 'thamani pungufu'
- Utekelezaji wa haki na adhima kwa mabinti waliopo ndani ya sekta nyeti kama vile kazi za kutoa huduma ya uangalizi, kazi za usafi, tasnia ya utumishi na malezi, kazi za kihisia na kazi za ndani
- Utambuzi wa mchango wa mabinti katika ujumla wake, ndani ya sehemu ya kazi na ndani ya utengenezaji wa sera, kulingana na ujuzi na vipaji vyetu, na si kulingana na jinsia, umri au wadhifa wa ndoa. Tuna ustadi na tunaweza kulingana na adili ya bidii zetu, ustahili, uerevu wa kihisia na uongozi wa wanawake
- Uhakikisho wa haki za mabinti katika upewaji wa malipo ya likizo ya baada ya kujifungua, bila kubaguliwa, kuwekewa vikwazo au kufutwa kazi
- Ukadirifu muhimu wa athari ya makazi ya muda au yasiyo salama, misaada ya kiserikali isiyo toshelevu ama yenye muenendo mbovu, kwenye uwezo wa mabinti wa kutafuta na kudumu katika kazi, pamoja na hatua madhubuti za kuhamasisha ajira zenye kipato kizuri na zinazoheshimika kwa mabinti.

***Imetosha!***

***Hakuna tena kufanya kazi zisizo na malipo na kutoa huduma bure***




ILANI YA BINTI
AFRIKA BEIJING+25




# DAI LA KUPIGA MARUFUKU UKATILI WA KIJINSIA

**Sisi, Mabinti wa Afrika, tunadai:**

- Upigwaji marufuku wa janga la Ukatili wa Kijinsia katika miundo yake yote hasa katika migogoro, kuhamishwa makazi na masuala ya ukatili wa binadamu yanayojumuisha uuwaji wa wanawake, ubakaji, mienendo ya uharibifu, ukeketwaji, ndoa za utotoni na ndoa zisizo za hiari, udhia wa kingono, kutumiwa vibaya kingono, matumizi mabaya kijamii na kiuchumi, uuzaji wa binadamu na miundo mingine yote ya ukatili.

- Utekelezaji wa sera za ziada ili kuzuia ukatili wa kingono na kijamii, pamoja na kuhakikisha kwamba kesi za unyanyasaji, ukatili na vitendo vibaya dhidi ya wanawake zinatambuliwa, zinachunguzwa na wahalifu kuhukumiwa.

- Utoaji wa msaada wa kisheria, kimwili na kisaikolojia, makazi na huduma za kitaalamu kwa mabinti waliopitia vitendo vibaya vya kijamii na miundo mingine ya ukatili

- Ugavi wa fedha za kusaidia utafiti na uvumbuzi wa vijana kwa ajili ya kupambana na suala la Ukatili wa Kijinsia

## *Imetosha!*

***Jamii lazima iwekwe huru dhidi ya Ukatili wa Kijinsia***

ILANI YA BINTI AFRIKA BEIJING+25

# DAI LA KUKOMESHA UBAGUZI WA KIJINSIA

**Sisi, Mabinti wa Afrika, tunadai:**

- Uanzishi wa mikakati ya kisheria inayoondoa miundo yote ya ubaguzi dhidi ya wasichana na mabinti kwa msingi wa jinsia yao, hadhi ya ndoa, rangi ya ngozi, uraia na urithi, au umri, ili kuhakikisha haki zao za kibinadamu na msingi wa uhuru

- Upatikanaji wa haki na unaoweza kumudiwa wa bidhaa, huduma za umma na fursa kwa mabinti waishio vijijini, mabinti wenye ulemavu, mabinti wanaotafuta hifadhi, mabinti wakimbizi na mabinti wahamiaji na wasio na makazi. Huduma hizi zinajumuisha upatikanaji wa ulinzi wa kijamii, maji ya kunywa, haki za urithi, chakula na lishe, makazi, ulezi wa watoto, miongoni mwa haki na huduma nyingine

- Uondoaji wa miundo yote ya ubaguzi dhidi ya mabinti hasa ule unaoathiri mabinti maskini na wengine wote waliopo katika mazingira hatarishi, jambo linaloweza kusababisha kuondelewa kwao katika ufanyaji maamuzi

- Ufikivu sawa katika umiliki wa ardhi na kuhakikisha uhuru wa kiuchumi na uwezeshwaji binafsi. Mabinti wanaopigana dhidi ya sheria, mila na mienendo inayowakandamiza wanawake, katika usimamizi wa urithi, na ile inayoingilia ufikivu sawa wa wanawake kwenye umiliki wa ardhi na rasilimali asilia

- Utoaji wa mifumo endelevu ya kifedha kwa mabinti wanaotafuta hifadhi na mabinti wakimbizi ili kuhakikisha riziki yao na ujumuishwaji mpya, pamoja na usalama wao na ustawi

***Imetosha!***

***Lazima tukomeshe ubaguzi wa kijinsia***




ILANI YA BINTI
AFRIKA BEIJING+25




# DAI LA UPATIKANAJI WA HAKI NA ULINZI

**Sisi, Mabinti wa Afrika, tunadai:**

- Mapitio, marekebisho au maboresho ya sheria zinazowakandamiza mabinti ili kuhakikisha kwamba kunakuwepo usawa katika uso wa sheria na ufikivu sawa wa haki. Hili hujumuisha, ila si tu, ulinzi wa haki za mabinti hasa katika vipindi vya mapigano yatumiayo silaha, majanga ya kiasili na upotevu wa makazi. Ni wajibu wa jamii ya kimataifa kushughulikia visababishi vikuu vya migogoro hii inayoathiri sana mabinti waliopo kwenye mazingira hatarishi

- Utoaji wa taarifa kuhusiana na haki za mabinti na wasichana katika namna inayoweza kufikika, ya uwazi na iliyo katika miundo na lugha inayoeleweka, pamoja na michakato na zana angavu na fanisi za kudai haki hizo ili kuhakikisha kwamba zinatekelezwa kikamilifu

- Utoaji wa elimu kupitia mafunzo, kampeni na programu za uamsho, kwa ajili ya wasichana na wavulana, familia, jamii na mfumo mzima wa uongozi wa kiserikali katika kulinda haki za mabinti na wasichana

- Ugavi wa kifedha ili kuimarisha uwezo wa mabinti kupitia ufikivu ulioboreshwa wa taarifa na usaidizi wa kisheria pasipo kujali hali na vizingiti vyao vya kijamii na uchumi

## *Imetosha!*

***Usawa & Haki mbele ya Sheria***

ILANI YA BINTI
AFRIKA BEIJING+25

# DAI LA HAKI ZA AFYA YA KIJINSIA NA UZAZI

**Sisi, Mabinti wa Afrika, tunadai:**

- Upatikanaji wa haki na huduma muhimu za kimataifa za afya ya kijinsia na uzazi hasa kwa wale waliopo maeneo ya vijijini, ijumuishayo ushauri nasaha kwa mabinti kuhusiana na uhuru wao wa kijinsia na uzazi. Afya yetu ya uzazi si jambo la aibu, usumbufu, au sababu ya kubaguliwa.

- Utambulishi na utekelezaji wa kozi na programu fanisi za Elimu ya Kina ya Jinsia mashuleni ili kuelimisha mabinti juu ya afya zao na namna maamuzi yao yanaweza kuathiri ustawi wao na wa watu wengine. Kama mabinti, tuna haki ya kuongoza miili yetu wenyewe, kufanya maamuzi kwa uhuru na kwa kuwajibika, kuhusiana na masuala yanayohusiana na uhuru wetu wa kijinsia, ubaguzi na ukatili

- Uondoaji wa kodi katika bidhaa za hedhi, utekelezaji wa sera endelevu za vipindi vya hedhi kwenye maeneo yote ya kazi, na utoaji wa pedi bure na zana za usafi ndani ya shule zote. Ni jambo lisilokubalika kabisa mwaka 2020 kwamba wasichana waache shule au kupoteza ajira zao kwa sababu tu ya hedhi zao

- Kutoa misaada ya kifedha kwa taasisi zinazotoa muongozo wa taarifa na programu za elimu ya kina ya masuala nyeti ya kijinsia, elimu ya afya ya jinsia na uzazi, na uwezeshaji wa ustawi wa mabinti

***Imetosha!***

***Miili Yetu, Chaguzi Zetu!***




ILANI YA BINTI
AFRIKA BEIJING+25




ILANI YA BINTI
AFRIKA BEIJING+25

# DAI LA AFYA YA AKILI NA USTAWI

**Sisi, Mabinti ya Afrika, tunadai:**

- Utoaji wa huduma za afya ya akili zinazoelewa athari ya ubaguzi wa kijinsia, chuki na unyanyasaji unaosababisha changamoto kubwa zinazoathiri afya ya kiakili ya mabinti

- Utengenezaji na utekelezaji wa sera, huduma na mienendo inayoshughulikia changamoto za afya ya kiakili, zilizotengenezwa kwa kuzingatia mapito halisi ya mabinti na kufaa mahitaji yao binafsi

- Utekelezaji wa mabadilisho ya kimfumo na uundwaji mpya wa mifumo ili kuboresha uwasilishwaji wa huduma inayohusiana na afya ya kiakili, ushauri nasaha, msaada wa kutatua mfadhaiko, kwa kutumia mkakati makini, unaozingatia jinsia, na kulenga vijana

- Uondoaji wa vizingiti vyote vinavyoweza kuwa na athari mbaya katika ujumuishwaji mkamilifu wa vijana wenye changamoto za kiakili na kimwili ndani ya jamii, ikiwa ni pamoja na utoaji wa miundombinu na huduma sahihi za kuwezesha ujumuishwaji na upatikanaji sawa wa fursa, bila kuwepo kwa ubaguzi wowote

- Fedha kwa ajili ya huduma endelevu na ya usawa ya afya ya kiakili. Matatizo ya kiakili yanachangia sehemu kubwa na inayokua ya mzigo wa magonjwa wa bara hili, hatahivyo bado hubaki kupewa kipaumbele kidogo sana katika uwezeshwaji wa umma kifedha ndani ya mifumo ya afya

## *Imetosha!*

***Huduma ya afya ya kiakili sharti ipatikane kote na kwa usalama***

# DAI LA ELIMU JUMUISHI, YENYE USAWA NA YENYE UBORA

**Sisi, Mabinti wa Afrika, tunadai:**

- Kuongezeka kwa mgao wa bajeti ya kitaifa kwenye elimu (na kupunguza ile ya matumizi ya kijeshi) ili kuchochea mifumo ya mafunzo ya kieletroniki katika uwasilishaji wa elimu yenye ubora, jumuishi na itolewayo bure, ya awali, msingi, sekondari na elimu ya juu hasa kwa mabinti na wasichana waliopo maeneo ya mashambani

- Uondolewaji wa vizingiti katika elimu ya mabinti na wasichana, vinavyojumuisha umaskini, ada za shule, usafiri, umbali na usalama wa shule, ndoa za utotoni na ushurutishwaji wa ndoa, mimba za utotoni na zisizotarajiwa, ukosefu wa nyenzo za usafi na za uhifadhi wa hedhi, upendeleo wa kijinsia na dhana potofu kiujumla, nyenzo za kujifunzia na michakato ya elimu, uonevu, vitendo ovu na ukatili mashuleni, vyuo vya awali na vyuo vikuu

- Taasisi zinazotoa elimu kwa wavulana kuhusu kuwaheshimu wasichana na kuenenda nao kwa usawa, huku wakielewa asili ya mfumo dume yenye mahusiano yasiyo na usawa katika uongozi, wajibu na dhana za kijinsia

- Uhakikisho wa upatikanaji na ufikivu wa usawa katika uhitimu wa shule za ufundi, sekondari na elimu ya juu, ili kutatua kwa ufanisi ukosefu wa usawa uliopo baina ya vijana wa kiume na wa kike katika taaluma fulani

- Uwezeshwaji wa mabinti wanaotoka kwenye jamii hatarishi na zilizotengwa, mazingira ya migogoro na ya misaada ya kibinadamu, na kuwapatia nafasi sawa za kujiunga na vyuo vikuu bora kupitia huduma ya ufadhili hasa katika Sayansi, Teknolojia, Uhandisi na Hisabati

## *Imetosha!*

***Elimu ni haki, si pendeleo***




ILANI YA BINTI
AFRIKA BEIJING+25




# DAI LA HAKI YA KIDIGITALI

**Sisi, Mabinti wa Afrika, tunadai:**

- Uongezaji wa kasi katika mageuzi ya kidigitali hasa kwa mabinti waliopo vijijini na maeneo hatarishi, ikiwa ni pamoja na upatikanaji rahisi wa intaneti, inayoweza kumudiwa na kutegemeka, pamoja na uwekezaji katika miundombinu na teknolojia zinazowezesha uchumi wa kidigitali na fursa mpya kwa mabinti

- Upigwaji marufuku wa vizuizi vilivyopitiliza kiasi katika uhuru wa intaneti na kufungwa kwa intaneti

- Demokrasia katika Nyanja ya kidigitali ili kuruhusu uchangizi na ushiriki sawa kwani mabinti wengi huachwa nyuma katika mageuzi ya kidigitali

- Ulinzi dhidi ya udhalilishwaji wa kupitia mitandao ya intaneti, vitisho na lugha za ubaguzi wa kijinsia zinazojaribu kuwanyamazisha mabinti katika kueleza maoni yao, na kuwanyima haki yao kamili ya kustawisha utu wao wa kidigitali, na ushiriki wao katika mahojiano ya kijamii, kitamaduni na kisiasa

## *Imetosha!*

***Heshimu utu wetu wa kidigitali.***

## DAI LA KUNYAMAZISHA

# BUNDUKI

**Sisi, Mabinti wa Afrika, tunadai:**

- Ulinzi wa haki za mabinti na uwajibishwaji katika vipindi vya mapigano yatumiayo silaha, uchukuaji wa maeneo, majanga ya kiasili na dharura za kibinadamu. Sisi, kama mabinti, hatuzalishi, kuuza wala kununua bunduki, sasa kwanini tunalazimika kulipa gharama ya wababe wa vita?

- Ulinzi wa haki ya mabinti katika kushiriki maandamano ya amani, mikutano na uhuru wa kujieleza pamoja na utekelezaji wa sera na michakato ya kuchunguza ukatili wa polisi na manyanyaso dhidi ya wanawake na haki nyinginezo za kibinadamu katika kipindi cha janga lililopo na siku zote zijazo

- Urasimishaji wa ushiriki wa mabinti katika jitihada na michakato ya kujenga amani, upatanishi na mazungumzo, huku michango yao ikinakiliwa

- Ugavi wa fedha na usaidizi kwa mabinti, taasisi, programu maalum za mabinti za ujenzi wa amani ndani ya makutano ya ajenda za kati ya Vijana, Amani na Usalama, Wanawake Amani na Usalama

## *Imetosha!*

***Afrika Tunayoitaka ni Ile Isiyo na Migogoro***




ILANI YA BINTI
AFRIKA BEIJING+25




# DAI LA UJUMUISHWAJI KATIKA UONGOZI WA PAMOJA

**Sisi, Mabinti wa Afrika, tunadai:**

- Urasimishwaji wa uongozi kwa ajili ya ushirikishwaji mkamilifu na fanisi wa mabinti, katika siasa, na fursa sawa za uongozi katika ngazi zote za ufanyaji maamuzi ndani ya nyanja za kisiasa, kijamii, kitamaduni, kiuchumi na kiraia maishani, huku zikiimarisha sauti za mabinti na kutengeneza rasilimali kwa ajili ya ajenda zao

- Utekelezaji wa upigaji kura wa mabinti ndani ya kura za wanawake na vijana. Hatujui tuko wapi ndani ya mifumo ya sera, kura za vijana na takwimu za kijinsia hazijaweza bayana nafasi ya wanawake, haki na ushiriki wao

- Uteuzi wa mabinti wataalamu na Washauri Maalum/Wajumbe na nafasi nyingine katika tasnia, taasisi na kila ngazi ya kitaifa, kikanda na uongozi za kimataifa

- Utengenezaji wa jukwaa endelevu za majadiliano kwa ajili ya kuimarisha mitandao ya Pan-African na ujumuishwaji wa mabinti na wanawake katika mafunzo, ushirikishaji, ushauri, ushikamano na uwezeshaji

# Imetosha!

***Ni muda wa kuongoza pamoja sasa***

ILANI YA BINTI
AFRIKA BEIJING+25

## *Imetengenezwa na*

African Union Youth Envoy

## *Imeungwa mkono na*

ILANI YA BINTI
AFRIKA BEIJING+25